MAAZIMIO YA MKUTANO WA WADAU WA SEKTA YA UVUVI ULIYOFANYIKA KWENYE UKUMBI WA CHUO CHA BENKI KUU, MWANZA KUANZIA TAREHE 16–18 DESEMBA, 2009

UTANGULIZI

Tanzania inamiliki maeneo makubwa ya maji ambamo rasilimali za uvuvi hupatikana kwa wingi. Maeneo hayo ni pamoja na Ziwa Vctoria, Ziwa Tanganyika Ziwa Nyasa, Mabwawa (Nyumba ya Mungu, Mtera na mengine mengi ya asili), mito (Rufiji, Ruvu, Kilombero n.k.), malambo na maeneo oevu ambayo yana fursa kubwa ya uvuvi hapa nchini. Aidha, kuna Bahari ya Hindi ambayo ina maeneo mawili ya Bahari ya Taifa (Territorial Sea) na Ukanda wa Uchumi wa Bahari (Exclusive Economic Zone - EEZ).

Sekta ya uvuvi inatoa mchango mkubwa katika kuwapatia wanachi ajira, lishe, kipato, na kuingizia nchi fedha za kigeni. Uvuvi nchini huendeshwa na wavuvi wadogo takriban 200,000 ambao huvua asilimia zaidi ya 90 ya samaki wote wanaovuliwa nchini. Zaidi ya wananchi 4,000,000 hujishughulisha na kujikimu kutokana na shughuli zinazoendana na uvuvi hapa nchini.

Takwimu za mwaka 2008 zinaonyesha kuwa sekta ya uvuvi ilikua kwa kiwango cha asilimia **5** na kuchangia kwenye Pato la Taifa (GDP) kwa asilimia **1.2** ikilinganishwa na mwaka 2007 ambapo ukuaji wa sekta ulikuwa asilimia **4.5** na mchango katika pato la Taifa asilimia **1.3.** Aidha, katika kipindi hicho, jumla ya tani **324,821** za samaki zilivuliwa zikiwa na thamani ya takriban Shilingi **bilioni 371.4** ikilinganishwa na tani **327,845** zilizovuliwa mwaka 2007 zikiwa na thamani ya Shilingi **bilioni 292**. Vilevile, katika mwaka 2008, jumla ya tani **51,426** za mazao ya uvuvi na samaki wa mapambo waliuzwa nje ya nchi kwa thamani ya Dola za Kimarekani **174.4 milioni.**

Usimamizi wa rasilimali za uvuvi hufanyika kwa kuzingatia Sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 1997 na Sheria ya Uvuvi Na. 22 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za mwaka 2009. Hata hivyo, usimamizi wa rasilimali za uvuvi unakabiliwa na **tatizo sugu la uvuvi haramu** unaondeshwa na baadhi ya wavuvi pasipo kuzingatia Sheria na Kanuni zilizopo.

Uvuvi haramu unaofanyika kwenye maji baridi ni pamoja na uvuvi wa kutumia makokoro, nyavu za macho madogo, nyavu za timba (monofilament), kimia (cast net), katuli, mikuki na uvuvi wa sumu. Athari kubwa inatokana na kukamata samaki wachanga, huharibu mazalio ya samaki, malisho na makulio ya samaki. Aidha, nyavu za macho madogo pia hukamata samaki wachanga, wakati nyavu za makila aina ya timba huendelea kuua samaki wakati wote. Pia upo uvuvi wa sumu ambao huua samaki pamoja na viumbe wengine na pia huharibu mazingira na ni hatari kwa afya za binadamu na viumbe wengine.

Uvuvi haramu unaofanyika katika Bahari ya Hindi ni pamoja na uvuvi wa mabomu, nyavu za macho madogo, kokoro, mtando/juya la kojani/juya la kusini, timba, mikuki, sumu, bunduki za kwenye maji/mitambo, mchokoo na uzamiaji wa kutumia mitungi ya gesi. Aidha, upo uharibifu wa matumbawe unaotokana na uvunaji kwa ajili ya kutengeneza chokaa na ukataji wa

mikoko. Uvuvi wa mabomu huharibu matumbawe ambayo ni mazalia, malisho, maficho na makazi ya samaki na viumbe. Hali kadhalika, upo uporaji wa rasilimali ya uvuvi, hususan katika eneo la EEZ ambao hufanywa na meli za kigeni. Uvuvi wa mabomu husababisha vifo na ulemavu kwa binadamu wanaojihusisha na uvuvi huo. Ifahamike kuwa matumbawe huchukua takriban miaka 70 hadi 100 kujijenga upya tena.

Kutokana na uharibifu uliopo katika uvuvi umesababisha kuwepo kwa upungufu mkubwa wa rasilimali ya uvuvi, hususan katika Ziwa Victoria ambalo huongoza kwa upatikanaji wa samaki aina ya Sangara ambao wamepungua kutoka **tani 676,000** mwaka 2006 hadi **tani 331,000** mwaka 2009. Hali hii imetokana na sababu zifuatazo:-

- Ongezeko la kasi ya matumizi ya zana haramu pamoja na ongezeko la idadi ya wavuvi kutoka **92,529** mwaka 2000 hadi **105,016** mwaka 2008;
- Ongezeko la vyombo vya kuvulia samaki kutoka vyombo **30,171** (2000) hadi vyombo **52,174** (2008); na
- Ongezeko kubwa la mahitaji ya samaki na mazao yake katika soko la samaki ndani na nje ya nchi na hivyo kuwa kichocheo kikubwa cha samaki wachanga kuvuliwa. Kwa upande wa Bahari ya Hindi, mathalani rasilimali ya kambamiti imepungua kiasi cha kusababisha uvuvi wake kwa meli kubwa kufungwa hadi sasa. Aidha, rasilimali ya Kambamiti (*Prawns*) imepungua kutoka **tani 1,320** kwa mwaka 2003 hadi kufikia **tani 205** mwaka 2007.

Madhara yatokanayo na uvuvi haramu katika Bahari ni pamoja na:

- Kupungua kwa bionuai mfano, samaki aina ya pweza, kambamiti, kambakochi na jongoo bahari. Pia, aina nne za makombe (Cypraecassis rufa, Cassis cornuta, Tridac na spp);
- Bahari kuwa jangwa kutokana na uharibifu wa matumbawe, majani bahari, maeneo ya mikoko na sakafu ya bahari; na
- Kumomonyoka fukwe za bahari na uchafuzi wa maji na kuharibu ikolojia kwenye maji.

Kutokana na kukithiri kwa matumizi ya zana haribifu biashara haramu katika uvuvi na utoroshaji na uporaji wa rasilimali za uvuvi nchini, Serikali inalazimika kutoa maamuzi yatakayonusuru rasilimali zetu kwa ajili ya maendeleo na manufaa ya wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kutoa tamko lifuatalo ili kulinda rasilimali ya uvuvi kwa ajili ya kizazi cha sasa na kijacho.

Azimio:
Kwa kuzingatia madhara makubwa yatokanayo na uvuvi haramu, Serikali itoe Tamko kuwa itachukua hatua kali mara moja kutokomeza uvuvi haramu hapa nchini. Wadau wanapendekeza kuwa tamko litolewe na viongozi Wakuu wa Nchi; - Rais/Makamu wa Rais/ Waziri Mkuu.

Pamoja na tamko hilo maazimio mengine yaliyotolewa na wajumbe wa Mkutano wa Wadau wa Sekta ya Uvuvi ni kama ifuatavyo:

Na.	HOJA	AZIMIO	MUDA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
1.	Kutokomeza uvuvi na biashara haramu	1.1 Viongozi wa Serikali, Vyama vya Siasa na Watendaji wote katika Serikali Kuu, Mikoa, Halmashauri, Serikali za Vijiji, Beach Management Units (BMUs) na wadau wa uvuvi wahusike kikamilifu katika kudhibiti uvuvi na biashara haramu.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Wizara ya Katiba na Sheria; Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; OWM-TAMISEMI; Mikoa, Wilaya, Halmashauri, Vyama vya Siasa, na wadau wengine.
		1.2. Viongozi pamoja na watumishi wa umma wanaojihusisha na uvuvi na biashara haramu wachukuliwe hatua za kisheria na kinidhamu.	Kuanzia sasa na kuendelea	Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma; OWM-TAMISEMI; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Wizara ya Katiba na Sheria; Mikoa, Wilaya, Halmashauri na Vyama vya Siasa.
		1.3. Elimu ya uvuvi endelevu itolewe kwa wavuvi, wawekezaji, vyombo vya dola na wadau wengine.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Katiba na Sheria; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; OWM-TAMISEMI; Mikoa, Wilaya, Halmashauri, Sekta Binafsi, NGOs na BMUs.
		1.4. Utengenezaji, uingizaji na uuzaji wa zana haramu za uvuvi udhibitiwe.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; Wizara ya Fedha na Uchumi; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; TRA, Mikoa, Wilaya, Halmashauri, Wavuvi na BMUs.
		1.5. Viwanda na maduka yanayouza zana za uvuvi yakaguliwe mara kwa mara na hatua stahili zichukuliwe.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; Wizara ya Fedha na Uchumi; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; TRA, Mikoa, Wilaya na Halmashauri.

Na.	HOJA	AZIMIO	MUDA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
		1.6. Utafiti ufanyike ili kubaini kiwango cha athari zinazotokana na uvuvi haramu na matokeo yarejeshwe kwa jamii na wadau wengine.	2010 na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, TAFIRI, COSTECH, Vyuo Vikuu, wavuvi na wadau wengine.
		1.7. Mikoa, Wilaya, Halmashauri na sekta binafsi ziwe na utaratibu wa kuwa na mikutano ya kufanya tathmini ya maendeleo ya sekta ya uvuvi. Aidha, taarifa za Mikoa, Wilaya na Halmashauri zijumuishe masuala ya uvuvi.	Kuanzia sasa na kuendela	OWM- TAMISEMI; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Mikoa, Wilaya na Halmashauri.
		1.8. Mahakama ziharakishe kutoa hukumu za kesi zinazohusu uvuvi na biashara haramu ya mazao ya uvuvi.	2010 - 2011	Wizara ya Katiba na Sheria; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Mikoa, Wilaya, Halmashauri na BMUs.
		1.9. Kiundwe kikosi maalumu cha doria kwa ajili ya kulinda wavuvi na rasilimali za uvuvi kwenye EEZ na maeneo mengine ya uvuvi	Kuanzia sasa na kuendelea	OR- Menejimenti ya Utumishi wa Umma; OWM-TAMISEMI; SMZ; Wizara ya Fedha na Uchumi; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; na Wizara ya Katiba na Sheria.
		1.10. Kushirikisha nchi jirani katika kudhibiti uvuvi na biashara haramu	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki; Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Wizara ya Fedha na Uchumi; Mikoa, Wilaya na Halmashauri.

Na.	HOJA	AZIMIO	MUDA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
2.	Huduma za Utafiti, Mafunzo na Ugani	2.1 Serikali iimarishe Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI).	2010-2013	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; na Wizara ya Fedha na Uchumi.
		2.2 Serikali iimarishe na kupanua vyuo vya mafunzo ya uvuvi.	2010 - 2013	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Fedha na Uchumi; Vyuo Vikuu; Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi; Wizara ya Kazi, Ajira na Maendeleo ya Vijana; Wizara ya Mawasilino, Sayansi na Teknolojia.
		2.3. Watumishi wa Ugani wapatiwe mafunzo rejea na vitendea kazi, ikiwemo vyombo vya usafiri.	2010 - 2013	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; OWM- TAMISEMI na Halmashauri.
		2.4. Ili kutekeleza azma ya **Kilimo Kwanza**, pale ambapo kuna uhaba wa wataalam wa Sekta ya Uvuvi, viongozi na wataalam wa halmashauri wapatiwe mafunzo ya msingi kuhusu masuala ya uvuvi ili waweze kufanya kazi za ugani.	2010 na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; OWM-TAMISEMI Halmashauri na wadau wengine.
		2.5. Wataalam wanaohitimu kwenye vyuo vya uvuvi waajiriwe na Halmashauri moja kwa moja kama ilivyo kwa sekta za kilimo, mifugo, elimu na afya.	Kuanzia sasa na kuendelea	OR- Menejimenti ya Utumishi wa Umma; OWM-TAMISEMI; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; na Halmashauri.
		2.6. Majukumu ya watendaji wa Sekta ya Uvuvi ngazi ya Halmashauri yazingatiwe kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu.	Kuanzia sasa na kuendelea	OWM-TAMISEMI; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Mikoa, Wilaya na Halmashauri.
		2.7 Sekretarieti za Mikoa ziunde ikama ili ziweze kuajiri wataalamu wa uvuvi kwa lengo la kusimamia	Kuanzia sasa na kuendelea	OR- Menejimenti ya Utumishi wa Umma; OWM-TAMISEMI; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; na Mikoa.

Na.	HOJA	AZIMIO	MUDA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
		masuala ya uvuvi katika Mkoa.		
		2.8. Mikoa na Wilaya ziwe na mipango ya pamoja ya kusimamia rasilimali za uvuvi kwenye maeneo ya maji wanayochangia katika matumizi (Bahari, Maziwa, Mabwawa na Mito).	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Mikoa na Halmashauri husika.
		2.9. Kutokana na umuhimu wa sekta ya uvuvi kwa wananchi hususan vijijini, Halmashauri zitenge fedha za kutosha za kutekeleza huduma za ugani.	Kuanzia sasa na kuendelea	OWM-TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Mikoa na Halmashauri.
3.	Kuongeza mchango wa Sekta ya Uvuvi kwenye pato la Taifa (GDP)	3.1. Serikali itenge bajeti itakayokidhi mahitaji kwa ajili ya kutekeleza mipango ya kuendeleza Sekta ya Uvuvi.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Fedha na Uchumi; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; OWM-TAMISEMI na Halmashauri.
		3.2. Mfuko wa Kuendeleza Sekta ya Uvuvi uanzishwe	2010 na kuendelea	Wizara ya Fedha na Uchumi; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; na Halmashauri.
		3.3. Mifuko ya fedha iliyopo kwa ajili ya maendeleo ya jamii kama TASAF, SELF n.k itumike pia kugharamia miradi ya uvuvi.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Fedha na Uchumi; OWM-TAMISEMI, Mikoa, Wilaya na Halmashauri.
		3.4. Utalii-ikolojia kwenye maeneo ya maji uendelezwe na maeneo mapya ya utalii huo yaainishwe, yatengwe na yaendelezwe.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Maliasili na Utalii; Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU).
		3.5. Bandari za Uvuvi zijengwe kwenye maeneo yenye sifa kwa	2010 na kuendelea	Wizara ya Miundombinu; Wizara ya Fedha na Uchumi; Wizara ya Maji na

Na.	HOJA	AZIMIO	MUDA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
		lengo la kutoa huduma kwa wavuvi na kuvutia uwekezaji. Miundombinu ya kuwezesha bandari hizo ijengwe na kuboreshwa.		Umwagiliaji, Wizara ya Nishati na Madini; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; OMR- Mazingira; Washirika wa Maendeleo na wawekezaji.
		3.6. Taasisi za fedha zihamasishwe kutoa mikopo ya masharti nafuu katika kukuza sekta ya uvuvi.	2010 na kuendelea	Wizara ya Fedha na Uchumi; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; na OWM-TAMISEMI; Wizara ya Viwanda Biashara na Masoko; Mikoa, Wilaya na Halmashauri.
4.	Kuzingatia ubora na usalama wa mazao ya uvuvi.	4.1 Kuboresha Maabara ya Taifa ya Uvuvi Nyegezi na kujenga nyingine kwa ukanda wa pwani.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Fedha na Uchumi; na Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi.
		4.2 Kuongeza wataalam wa ukaguzi wa mazao ya uvuvi.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; OWM-TAMISEMI, Mikoa na Halmashauri.
5.	Kuboresha maisha ya wavuvi	5.1. Serikali za vijiji kwa kushirikiana na Halmashauri zitenge maeneo ya shughuli za uvuvi na kuweka huduma za msingi.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; OWM-TAMISEMI, Mikoa, Wilaya, Halmashauri, Serikali za Vijiji, BMUs na wavuvi.
		5.2. Kuhamasisha uanzishwaji wa ushirika wa wavuvi ikiwa ni pamoja na kupitia mitandao ya BMUs. Aidha, BMU zianzishwe na kuimarishwa nchi nzima na zitambuliwe na Halmashauri kupitia sheria ndogo zitakazotungwa na Halmashauri.	Kuanzia sasa na kuendelea	OWM-TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika, Mikoa, Wilaya, Halmashauri, BMUs na NGOs.
		5.3. Mialo iboreshwe na iendeshwe na BMUs chini ya usimamizi wa	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; OWM- TAMISEMI, Wizara ya

Na.	HOJA	AZIMIO	MUDA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
		Halmashauri.		Fedha na Uchumi; Mikoa, Halmashauri, BMUs na wadau wengine.
		5.4. Huduma za kibenki zitolewe kwa jamii ya wavuvi kwenye maeneo yao kwa ajili ya usalama wa fedha zao.	Wakati wote	OWM-TAMISEMI; Wizara ya Mifugo na Uvuvi; Taasisi za fedha.
		5.5. Serikali kwa kushirikiana na wadau wa sekta ya uvuvi iweke mazingira ya kuvutia uwekezaji wa ndani kwenye sekta ya uvuvi, hususan masuala ya kodi, miundombinu n.k	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Fedha na Uchumi; Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; TIC na TIFPA.
6.	Kuendeleza ukuzaji viumbe kwenye maji	6.1. Utafiti ufanyike ili kutambua maeneo yanayofaa kwa ajili ya ukuzaji viumbe kwenye maji na kutambua aina mbalimbali za viumbe wanaofaa kufugwa bila kuathiri mazingira na kuleta madhara kwa jamii.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; OMR- Mazingira; Vyuo Vikuu, NEMC; TAFIRI; Mikoa, Wilaya na Halmashauri.
		6.2. Vituo vya kuzalisha mbegu na kutotoa vifaranga vya samaki (hatchery) na vitalu vya mbegu za mwani viimarishwe na kuanzisha vipya.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; TAFIRI, Vyuo Vikuu, Sekta Binafsi, Mikoa na Halmashauri.
		6.3. Wawekezaji wahamasishwe kutengeneza vyakula bora vya samaki kwa ajili ya kuendeleza ukuzaji wa viumbe kwenye maji.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Kilimo, Chakula na Ushirika; Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; TIC, TBS na sekta binafsi.
		6.4. Mafunzo ya ukuzaji viumbe kwenye maji yatolewe ili kujenga	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Halmashauri Serikali za Vijiji na

Na.	HOJA	AZIMIO	MUDA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
		uwezo kwa jamii na kila Halmashauri iwe na shamba darasa.		wakuzaji viumbe kwenye maji.
		6.5. Wawekezaji wahamasishwe kuweka miundombinu, hususan maji, umeme na barabara kwenye maeneo ya ukuzaji viumbe kwenye maji.	Kuanzia sasa na kuendelea	OWM-TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Wizara ya Nishati na Madini; Wizara ya Miundombinu; Wizara ya Fedha na Uchumi; Mikoa, Wilaya, Halmashauri, na Sekta binafsi.
		6.6. Kuimarisha kilimo na kukuza soko la zao la mwani	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; Wizara ya Fedha na Uchumi; OWM-TAMISEMI, Mikoa, Halmashauri, sekta binafsi, NGOs na wakulima.
7.	Upatikanaji wa takwimu sahihi za Uvuvi	7.1. Ukusanyaji takwimu katika Halmashauri uimarishwe kwa kuajiri watumishi wa Sekta ya Uvuvi, na kutoa mafunzo kwa wavuvi na wadau wengine na kwa kutumia (format) iliyopo katika kupanga na kutekeleza mipango ya Sekta.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Viwanda Bisahara na Masoko; Wizara ya Fedha na Uchumi; TRA, Mikoa, Halmashauri, BMUs, wavuvi, sekta binafsi na wadau wengine.
		7.2. Halmashauri zihakikishe kuwa wavuvi wanashusha samaki kwenye mialo rasmi.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; OWM-TAMISEMI, Mikoa, Wilaya, Halmashauri, Serikali za Vijiji, BMUs, wavuvi na wadau wengine.
8.	Kuimarisha biashara ya mazao ya uvuvi	8.1. Wavuvi wahamasishwe kufanya biashara ya ushindani moja kwa moja na wenye viwanda badala ya kutumia mawakala.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi. Wizara ya Fedha na Uchumi, Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, Mikoa, Wilaya, Halmashauri, sekta binafsi, wavuvi na BMUs.
		8.2. Wafanyabiasha na wavuvi	Kuanzia sasa na	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na

Na.	HOJA	AZIMIO	MUDA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
		wanatakiwa kuzingatia taratibu, masharti na matakwa ya soko.	kuendelea	Uvuvi; Wizara ya Biashara na Masoko; Wizara Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; TBS, Mikoa, Wilaya na Halmashauri.
		8.3. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi na hususan wamiliki wa viwanda vya kusindika samaki iimarishe kiwanja cha Mwanza ili ndege kubwa ziweze kutua na kubeba mazao ya uvuvi kutoka Ziwa Victoria.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; Fedha na Uchumi; TRA; Wizara ya Miundombinu; Wizara ya Nishati na Madini; Wizara ya Maji na Umwagiliaji; Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Mikoa, Wilaya, Halmashauri na sekta binafsi.
9.	Kupunguza kiwango cha upotevu wa mazao ya uvuvi kabla ya kumfikia mlaji	9.1. Wavuvi, wafanyabiashara na wenye viwanda vya samaki wapewe mafunzo ya kuboresha uchakataji wa mazao ya uvuvi.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wamiliki wa Viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi, Mikoa, Halmashauri, SIDO, NGOs, TIFPA na wadau wengine.
		9.2. Biashara ya samaki wachanga katika maeneo mbalimbali ikomeshwe.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi; Wizara ya Katiba na Sheria; TRA, Mikoa, Wilaya, Halmashauri, Serikali za Vijiji, wavuvi, BMU na wadau wengine.
10.	Matatizo yanayokabili Maziwa nchini.	10.1. Serikali ya Tanzania ishirikiane na Serikali ya Malawi kutatua tatizo la mpaka katika Ziwa Nyasa.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi.
		10.2. Hatua za haraka na za makusudi zichukuliwe ili kunusuru maziwa, mabwawa na mito inayokauka ikiwa ni pamoja na Ziwa	Kuanzia sasa na kuendelea	OMR- Mazingira, OWM-TAMISEMI, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maliasili na Utalii, Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mikoa,

Na.	HOJA	AZIMIO	MUDA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
		Jipe, Ziwa Manyara na Ziwa Rukwa n.k.		Wilaya, Halmashauri na wadau wengine.
11.	Upatikanaji wa zana bora na pembejeo za uvuvi.	Serikali itoe ruzuku ya zana bora na pembejeo za uvuvi.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Fedha na Uchumi; Wizara ya Viwanda na Biashara, TRA, Mikoa, Wilaya na Halmashauri.
12.	Masuala mtambuka.	Mipango ya uendelezaji uvuvi iainishe na kujumuisha masuala mtambuka ikiwa ni pamoja na masuala ya Jinsia, Ukimwi, Mazingira, Mabadiliko ya tabia nchi (climate change), ukiukwaji wa haki za binadamu (unyanyasaji wa kijinsia, kufanyisha watoto wadogo kazi).	2010 na kuendelea	Ofisi ya Makamu wa Rais; OWM-TAMISEMI, TACAIDS, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; NEMC, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto; Washirika wa Maendeleo, NGOs, Mikoa, Wilaya na Halmashauri.
13.	Uimarishaji na usimamizi wa maeneo ya mazalia ya samaki na maeneo tengefu	13.1. Maeneo ya mazalia ya samaki yatambuliwe, yatangazwe na yahifadhiwe.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Maliasili na Utalii; TAFIRI, Vyuo Vikuu, Mikoa, Wilaya na Halmashauri.
		13.2. Maeneo tengefu mapya na hifadhi kwenye maji ziainishwe na ziendelezwe.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maliasili na Utalii, TAFIRI, Vyuo Vikuu, MPRU, Mikoa Halmashauri.
14.	Kuimarisha biashara ya samaki wa mapambo	Rasilimali ya samaki wa mapambo itathminiwe na kuhamasisha uwekezaji katika biashara hiyo.	Kuanzia sasa na kuendelea	Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko; Wizara ya Fedha na Uchumi; TIC, sekta binafsi, Taasisi za Fedha, TAFIRI, Vyuo Vikuu, Mikoa, Wilaya, Halmashauri na wadau wengine.

Na.	HOJA	AZIMIO	MUDA UTEKELEZAJI	MHUSIKA
15.	Ushirikishwaji wa Chama Tawala, vyama vingine vya siasa, Bunge na madiwani	15.1. Chama Tawala, Vyama vingine vya siasa, Asasi za kijamii, Taasisi za kidini na Mashirika yasiyo ya kiserikali vihamasishe utekelezaji wa mipango inayolenga kuleta mapinduzi katika sekta ya uvuvi.	Kuanzia sasa na kuendelea	Ofisi ya Waziri Mkuu, Chama Tawala, Vyama vingine vya siasa, CBOs na NGOs.
		15.2. Kushirikisha Wabunge na Madiwani katika kutekeleza masuala ya Sekta ya Uvuvi.	Kuanzia sasa na kuendelea	Ofisi ya Waziri Mkuu, Ofisi ya Bunge; OWM- TAMISEMI; Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi; Mikoa, Wilaya, Halmashauri, Wabunge na Madiwani.